**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA.**
CHUO CHA UALIMU VIKINDU
**S.L.P.16268, Dar es Salaam.**
**Barua pepe:** vikindutc@gmail.com
: +255 754752950/0645137237

KUMB.NA.VTC/SA/6/VOL.XI/129

NDG......................................................................

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

### 1.0. UTANGULIZI

Chuo cha Ualimu Vikindu ni miongoni mwa vyuo vya ualimu vya Serikali vilivyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kinapatikana mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mkuranga katika Kijiji cha Vikindu jirani na Wilaya ya Temeke kupitia barabara ya Kilwa. Chuo kinatoa kozi ya **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa sayansi ya jamii (kwa kutumia lugha ya Kiswahili)** muda wa mafunzo ni Miaka miwili (2) pamoja na **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi Kwa njia ya Masafa** kwa Muda wa mafunzo wa Miaka Mitatu (3).

#### 1.1. Kuchagulikuwa kujiunga

Ninayofuraha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi katika kozi ya .................................................................. .......................... kwa muda wa miaka .........

#### 1.2. KUFUNGUA CHUO

Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe **17/08/2026**. Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe husika kwa kuwa masomo yataanza mara moja. Fika chuoni na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa.

#### 1.3. NAMNA YA KUFIKA CHUONI.

Panda usafiri wowote utakao kufikisha Vikindu, kisha Shuka na fuata maelekezo ya bango la Chuo na Shule ya Msingi Vikindu, kiasi cha mita 800 hivi toka barabara kuu.

#### 1.4. MUHIMU

Ni vema kufika chuoni mapema kabla ya saa 10:00 jioni. Mwanachuo atapokelewa na kusajiliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi 10:30 Jioni kwa tarehe zilizopangwa.

#### 1.5. DIRA YA CHUO

Kuunganisha jitihada za wadau ili kuwezesha maadili na taaluma katika ufundishaji Kwa kuzingatia ubunifu na teknolojia ili kujenga jamii iliyo bora.

#### 1.6. DHAMIRA YA CHUO

Kuandaa walimu mahiri watakaoshiriki kuleta badiliko chanya kwa jamii ya kitaifa na Kimataifa.

#### 1.7. MOTTO WA CHUO – ELIMIKA UKAELIMISHE

## 2.0. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

### 2.1. Vyeti na vitambulisho

Ufikapo chuoni ripoti ofisi ya usajili ambapo utaonyesha:-

- Fomu ya maelekezo ya kujiunga na Mafunzo.
- Vyeti halisi (Original) vya kidato cha nne/sita, (Result slip) kwa wale ambao vyeti havijatoka) Pamoja na vyeti hivyo toa vivuli (photocopies) kwa matumizi ya ofisi.
- Iwapo umefanya mtihani wa kidato cha nne/sita kwa zaidi ya mkao mmoja njoo na vyeti vyote Pamoja na vivuli vyake.
- Cheti cha kuzaliwa (Original Birth Certificate) na kivulichake.
- Leaving certificate (Original) na kivulichake.
- Stakabadhi za malipo ya Ada na Michango ya Ek ulizolipia benki (Pay in slip).
- Picha mbili (2) passport size
- Cheti halisi (Original) cha Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali au msingi na kivuli chake.

**NB:-**

a) Kama huna **vyeti** tajwa usije kwani hutapokelewa kwa kukosa viambatisho hivyo muhimu.

b) Fomu ya kupimwa na Daktari wa serikali (medical Examination certificate) imeambatishwa (kwa wanachuo wa kozi ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi miaka miwili tu). Baada ya kuonyesha vitu vyote vilivyo tajwa hapo juu utaelekezwa ofisi ya Mhasibu na risiti zako ili usajiliwe rasmi. Huna haki ya kupata huduma ya chuo bila kulipa ada na michango Uliyoagizwa.

### 2.2. Ada na michango

a) **Ada ya Mafunzo kwa kozi zote ni** Tshs. 450,000/= kwa mwaka. Ada ilipwe kwa kutumia **'control Number'** ambayo kila mwanachuo atapewa na mhasibu. Namba ya simu ya mhasibu wa chuo ni 0718614915 au 0755764115. Usisahau kuandika Jina lako kamili

**i. Michango kwa wanachuo wa Astashada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa miaka miwili:-**

| S/N | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Usafi na mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Kukodisha godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 5 | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu |
| 6 | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Ulinzi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 8 | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **150,000/=** | |

**ii. Michango kwa wanachuo wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa njia ya masafa**

Mchango wa fedha za uendeshaji wa mafunzo ya masafa ni Tshs 150,000.00 kwa mwaka


Fedha za Michango yote zilipwe katika tawi lolote la **NMB** Ac/No.**22801000002**, Jina la akaunti ni **Vikindu TC Miradi ya Elimu na Kujitegemea.** Andika jina lako kamili.




CamScanner

## 2.3. SARE kwa wanachuo wa kozi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa miaka miwili

√ **WAVULANA-** Suruali mbili (2) nyeusi, (mshono umeambatishwa).
(Angalia mchoro hapo chini)



**WASICHANA** – Sketi mbili (2) nyeusi (mshono umembatishwa)
Sketi iwe ndefu, urefu uishie kati ya magoti na kisigino. Sketi hii haina Linda nyuma wa mpasuo. Sketi zinapatikana kwenye maduka yaliyo karibu na chuo kwa gharama ya shilingi 17,000/= kwa kila sketi. (Angalia mchoro hapo chini).




- ✓ Shati mbili kwa wote 'light blue' mikono mirefu.
- ✓ Mashati yanapatikana kwenye maduka yaliyo karibu na chuo kwa gharama ya shilingi 17,000/=kwa kila shati. Njoo na fedha kwa maelekezo zaidi (hii inaondoa hali ya kutofautiana kwa rangi za mashati).
- ✓ Tai ndefu nyeusi.
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi (wote) uje navyo.
- ✓ Koti jeusi mikono mirefu wote (uje nalo).
- ✓ Soksi nyeusi wote.
- ✓ T-shirt yenye kola na nembo ya chuo Tshs. 15,000/= inapatikana chuoni (Njoo na fedha taslim).
- ✓ Kitambaa cheusi (Hijab) waumini tu, kisiwe na urembo.
- ✓ NB:-**Pasi za umeme haziruhusiwi.**

**NGUO ZA MICHEZO**

- ✓ Track suit nyeusi yenye utepe mweupe. (Track trouser & track jacket)
- ✓ Bukta nyeusi moja.
- ✓ Raba za michezo.
- ✓ T-shirt moja nyeupe isiyo na kola.

**NB:**-Mwanachuo anunue na aje navyo.

## 2.4. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI

- ✓ Unatakiwa kuja na shuka mbili za rangi ya **Light blue.**
- ✓ Ndoo ndogo ya kuogea na galoni nyeupe ya lita tano ya maji ya kunywa .
- ✓ Mto mmoja.
- ✓ Chandarua nyeupe ya pembe nne.

## 2.5. CHAKULA

Chuo kinatoa chakula. Unatakiwa kuja na vyombo vya chakula (sahani, kikombe, Bakuli na kijiko). Chuo hakitoi chakula maalum.

### 3.0. MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA

Unatakiwa kuleta vifaa vyote vya taaluma ikiwa ni pamoja na madaftari 14, kalamu za wino, penseli, rula, mkebe wa hisabati, ream (photocopier paper) na begi la kubebea madaftari (vitakaguliwa).

### 4.0. MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA MWANACHUO

Chuo hakina zahanati, matibabu ya huduma ya kwanza yanapatikana chuoni. Ukitakiwa kutibiwa nje ya chuo, gharama za vipimo ni kwa mwanachuo. Kwa mwanachuo asiye na kitambulisho cha Bima ya Afya anapaswa kuchangia **Tshs. 50,400/=** ili aweze kupata huduma ya matibabu kwa muda wa mwaka mmoja. (Akiwa na miaka 21 aje na kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA). Fedha hizi zilipwe moja kwa moja kwa Mhasibu wa chuo na zitapelekwa NHIF Kibaha. Bima ya Afya ni **lazima** kwa kila mwanachuo. Alete picha moja (1) "passport size."

### 5.0. SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

Mwanachuo afikapo chuoni, atapitishwa kwenye sheria na taratibu za chuo (College rules and regulations). Vilevile atapewa fomu ya kujaza ili kukubaliana na taratibu hizo.

### 6.0. USAFIRI WA KUJA CHUONI NA KURUDI LIKIZO

Mwanachuo anatakiwa kugharamia nauli ya kuja chuoni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Chuo kikifungwa, kila mwanachuo anapaswa kurudi nyumbani.

### 7.0. MUHIMU

Tafadhali soma kwa makini maelezo haya kwa utekelezaji. Chuo hakipo tayari kwa usumbufu wowote. Aidha, stakabadhi halisi za malipo yote ziletwe chuoni kukatiwa risiti. Ni muhimu ikaandikwa jina la mwanachuo. Kumbuka kutochanganya ada na michango katika akaunti moja. Kila malipo yana akaunti yake.

### 8.0. MWISHO

Uongozi wa chuo unakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja chuoni. Ni matumaini yetu utazingatia kanuni, taratibu na sheria ili lengo litakalokuleta chuoni liweze kufikiwa.

## ELIMIKA UKAELIMISHE

## KARIBU SANA CHUONI VIKINDU

FFUrassa

______________________

FREDSON .F.URASSA

KAIMU MKUU WA CHUO

KAIMU Mkuu wa Chuo
Chuo cha Ualimu Vikindu
S.L.P 16208
DAR ES SALAAM

## GOVERNMENT OF TANZANIA

Part 'A'

To the Medical officer
………………………
………………………
………………………

Principal,
Vikindu Teacher s' College
P.O. BOX 16268
Dar es Salaam.

Re: Mr./Mrs . Miss ……………………………………………………………………
(Full name )

Please examine the above named to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course. The examination should include the following categories (I-III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy /category IV will also render also render a girl candidate ineligible for the course.

I. (a) Eye sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e ) Venereal diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
(h) Typhoid

II. Neuroses

III. Other serious diseases.

IV. Pregnancy

**NB:** The applicant will not be admitted unless this form is dully filled.

Mkuu wa Chuo
Chuo cha Ualimu Vikindu
S.L.P 16268
DAR ES SALAAM

Date:…08/06/2026…… Signature………………

## PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that He/She is physically fit/ unfit and mentally fit/unfit to a full time teacher course.

I. (a) Eye sight……………………………………………………………
(b) Hearing ……………………………………………………………
(c) Speech……………………………………………………………
(d) Limbs……………………………………………………………
(e )Venereal diseases……………………………………………………
(f) Leprosy……………………………………………………………
(g) Epilepsy……………………………………………………………
(h) Typhoid……………………………………………………………

II. Neuroses……………………………………………………………

III. Other serious diseases……………………………………………………

IV. Pregnancy……………………………………………………………

Date :……………………  Signature…………………

Station :……………………………… Designation:……………



CS CamScanner